# *Virusi vya Chikungunya*

DCHHS
Safe families, healthy lives.
Dallas County Health and Human Services

***Virusi vya Chikungunya ni nini?*** Virusi vya Chikungunya (CHIKV) vinasambazwa kwa watu kutoka kwa mbu. CHIKV husababisha homa kali na maumivu makali ya viungo yanayoanza ghafla. CHIKV mara nyingi havisababishi kifo, lakini dalili zinaweza kulemaza, na baadhi ya watu wanaweza kupata matatizo mabaya. CHIKV ni chanzo cha kuendelea kuelimika - si cha hofu. Kujifunza kuhusu virusi na njia za kuzuia maambukizi ni muhimu. Hatua unazochukua zinaweza kusaidia kukulinda dhidi ya magonjwa mengine yanayosambazwa na mbu, pia.

***CHIKV huenezwa vipi?*** CHIKV husambazwa kwa watu kupitia kuumwa na mbu haswa wakati wa mchana. Mbu huambukizwa wanaponyonya damu ya mtu ambaye tayari ameambukizwa virusi. Kisha mbu walioambukizwa wanaweza kueneza virusi kwa watu wengine kwa kuuma. CHIKV ni nadra kusambazwa kutoka kwa mama hadi mtoto mchanga wakati wa kujifungua. CHIKV havisambazwi kupitia mguso wa kawaida, kama vile kumgusa au kumbusu mtu aliye na virusi.

***Dalili za CHIKV ni zipi?*** Dalili huonekana kwa takriban siku 3 hadi 7 baada ya kuumwa na mbu aliyeambukizwa. Dalili za CHIKV hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, na zinaweza kujumuisha:

- Kuanza ghafla kwa homa kali (>102°F)
- Maumivu makali ya viungo haswa katika mikono na miguu
- Kichwa kuwanga
- Maumivu ya misuli
- Maumivu ya mgongo
- Upele (~50% ya kesi)

Wagonjwa wengi hupata nafuu baada ya siku au wiki chache.  Baadhi ya watu wanaweza kuwa na maumivu ya viungo ya muda mrefu. Matatizo huwa machache, lakini huwa maarufu sana kwa:

- Watoto wachanga (chini ya mwaka 1)
- Wazee (zaidi ya miaka 65)
- Watu walio na hali sugu kama vile kisukari, shinikizo la damu, n.k.

****Tahadhari inastahili kuchukuliwa na watu walio katika makundi haya ili kuepuka kuumwa na mbu.****

***CHIKV hutibiwa vipi?*** Hakuna dawa mahususi ya kutibu CHIKV na hakuna chanjo ya kuzuia CHIKV.

***Ninapaswa kufanya nini nikishuku kuwa nina CHIKV?*** Kutumia dawa (mbali na aspirini) ili kupunguza homa yako na maumivu ya viungo kunaweza kusaidia. Mwone daktari.

**Ukishuku kuwa huenda una CHIKV:**

- Rekodi dalili zako na umwone daktari.
- Jilinde dhidi ya kuumwa na mbu zaidi.
- Kama una CHIKV, kuepuka kuumwa na mbu kutawasaidia kuwalinda watu wengine kutokuwa wagonjwa.

***Ninaweza kufanya nini?*** **Jilinde kwa kutumia njia hizi 4.**

***DEET Siku Nzima Kila Siku***

Ukiwa nje, tumia vizuiaji vya wadudu vilivyo na DEET au vizuiaji vingine vya EPA vilivyoidhinishwa na ufuate maagizo.

***Vazi***

Valia nguo ndefu, isiyobana na inayong’aa nje.

***Kuondoa maji***

Ondoa maji yote yaliyotuama ndani na karibu na nyumbani kwako.

***Jioni na Alfajiri***

Punguza shughuli za nje wakati wa jioni na alfajiri mbu wanaposhughulika.